MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.21. Msimu wa Kilimo 2023/24* *Tathmini ya Aprili 21-30, 2024 na Matazamio kwa Kipindi cha Mei 1-10, 2024*

**MUHTASARI**

- Hali ya mvua inatarajiwa katika maeneo mengi nchini ambayo itasaidia ukuaji na maendeleo ya mazao
- Hali ya ukavu inayotarajiwa katika mikoa ya kanda ya kati (Dodoma na Singida) itasaidia kukomaa na kukauka kwa mazao hususan mahindi na alizeti
- Wafugaji wanashauriwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu hali ya mifugo na malisho ili kuweza kukabiliana na athari mbalimbali zinazoweza kujitokeza

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2024


Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliimarika kidogo wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu. Hali hii ilisababisha ukanda mvua (ITCZ) kusogea katika maeneo ya kaskazini mwa nchi.

Joto la bahari katika eneo kubwa la magharibi mwa Bahari ya Hindi lilikuwa la juu ya wastani ukilinganisha na eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi. Hali hii ilisababisha kuvuma kwa upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria, magharibi, nyanda za juu kusini magharibi, maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki na katika maeneo ya ukanda wa Pwani. Maeneo ya ukanda wa kati yalipata mvua nyepesi hadi za wastani

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2024

Katika kipindi hiki, maeneo mengi nchini yalipata mvua kiasi cha milimita (mm) 11 hadi mm 150 za mvua isipokuwa katika maeneo machache ya mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara, Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Ruvuma, Lindi, na Mtwara ambayo yalipata mvua chini ya milimita 11. Hata hivyo, maeneo machache ya mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, kusini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na kisiwa cha Unguja yalipata mvua zaidi ya milimita 150 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo.




Kielelezo 1: Kiasi cha mvua kwa siku kumi kwa kipindi cha Aprili 21-30, 2024

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2024

Katika dikadi hii, mvua zilizonyesha katika baadhi ya maeneo nchini zilisaidia ukuaji na maendeleo ya mazao. Hata hivyo, hali ya mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani iliathiri ukuaji wa mazao kwa baadhi ya maeneo.

Maeneo yanayopata mvua za Masika, mahindi yapo katika hatua ya kukua isipokuwa katika maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria ambako mahindi yapo katika hatua ya kukomaa.

Katika maeneo yanayopata mvua za Msimu hususan katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Dodoma, Mbeya, Iringa, Njombe, Ruvuma, na Rukwa, mahindi yapo katika hatua ya kukomaa.

Zao la alizeti lipo katika hatua ya kutoa maua hususan katika mikoa ya Morogoro na hatua ya kukomaa katika mikoa ya Singida na Dodoma.

Zao la mpunga lipo katika hatua ya kukomaa hususan kwa maeneo ya mikoa ya Rukwa, Tabora, Mbeya, Shinyanga na Morogoro na baadhi

ya wakulima katika mkoa wa Tabora waliendelea na uvunaji wa zao hilo.

Maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyama yalikuwa ya kutosha katika maeneo mengi nchini.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2024

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mabonde kimeendelea kuongezeka kutokana na mvua zinazoendelea.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2024

Migandamizo mikubwa mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kupungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kusogea kaskazini na kuwepo katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria.

Joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu ya wastani. Hali hii inatarajiwa kusababisha kutokea kwa mgandamizo mdogo wa hewa na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo ya jirani.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2024,

Maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na mikoa ya magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kuwa na mvua zitazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) zinatarajiwa kuwa na mvua katika maeneo machache hasa yale yenye miinuko.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani, na Dar es Salaam vikiwemo visiwa vya Unguja na Pemba) pamoja pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) zinatarajiwa kuwa na na inatarajiwa kuwa mvua na ngurumo za radi katika **baadhi ya maeneo.**

Maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara, na Kilimanjaro) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro) yanatarajiwa kuwa na mvua katika maeneo machache.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) inatarajiwa kuwa na hali ya ukavu kwa ujumla.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2024

Mvua zinazotarajiwa kunyesha katika maeneo mengi nchini zitasaidia kuongeza unyevunyevu katika udongo ambao utasaidia katika ukuaji na maendeleo ya mazao.

Hata hivyo, mvua inayotarajiwa katika maeneo mengi ya pwani ya kaskazini inaweza kuathiri ukuaji wa mazao kutokana na hali ya unyevunyevu wa udongo kupita kiasi na kutuama kwa maji mashambani. Wakulima wa maeneo hayo kwa kushauriana na maofisa ugani wanashauriwa kuchukua hatua stahiki za kudhibiti maji kutuama shambani na milipuko ya wadudu na magonjwa..

Hali ya ukavu inayotarajiwa katika mikoa ya kanda ya kati (Dodoma na Singida) itasaidia kukomaa na kukauka kwa mazao hususan mahindi na alizeti.

Kwa ujumla, wakulima wanashauriwa kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao ili kuweza kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na hali ya hewa inayotarajiwa, milipuko ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea pale vitakapojitokeza huku wakipata ushauri kutoka kwa maafisa kilimo katika maeneo yao.

Wavuvi wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya mabwawa ya ufugaji samaki, pia kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, hususan kwenye bahari ya Hindi na Maziwa Makuu ili kufanya maamuzi na mipango sahihi kwa ajili ya shughuli za uvuvi.

Wafugaji wanashauriwa kuhifadhi majani ya kutosha na kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2024

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka kutokana na mvua zinazotarajiwa.

Jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadaye.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: *www.meteo.go.tz*
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)